

**KATIBU MKUU KIONGOZI AKUTANA NA MKURUGENZI MKAZI WA BENKI YA  
DUNIA BIBI BELLA BIRD– 13 JANUARI, 2020**

Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Mhandisi, John W. H. Kijazi, leo tarehe 13 Januari, 2020 amekutana na Mkurugenzi Mkazi wa Benki ya Dunia, Bibi Bella Bird ofisini kwake Ikulu jijini Dar es Salaam kwa kikao kifupi ambapo pamoja na mambo mengine, Bibi Bird alichukua nafasi hiyo kumuaga rasmi Katibu Mkuu Kiongozi baada ya kumaliza muda wake kama Mkurugenzi Mkazi wa Benki hiyo kwa nchi za Tanzania, Malawi, Zambia, Msumbiji na Somalia.

Katika kikao hicho Bibi Bird alibainisha kuwa muda wake wa kuitumikia Benki hiyo nchini uliisha Juni, 2019 ila aliongezwa muda wa ziada na sasa anatarajia kuondoka rasmi tarehe 16 Januari, 2020 kwenda nchini Zambia na Msumbiji kwa ajili ya kuaga rasmi.

Mkurugenzi huyo ameelezea furaha yake kutokana na miradi mbalimbali inayoendelea nchini chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia, na pia alimshukuru Katibu Mkuu Kiongozi kwa ushirikiano wake hasa kutafuta majibu pale kunapokuwa na mkwamo katika utekelezaji wa miradi mbalimbali inayofadhiliwa na Benki hiyo hapa nchini. Aliahidi kuwa ataendelea kutoa ushirikiano kwa Tanzania akiwa makao makuu ya Benki hiyo jijini Washington DC, nchini Marekani, vilevile, ameahidi kuwa atamkabidhi ofisi Mkurugenzi mpya ambaye ana imani kuwa ataendeleza ushirikiano na Serikali ya Tanzania.

Naye Katibu Mkuu Kiongozi alimshukuru Bibi Bird kwa ushirikiano wake alioutoa kwa Serikali ya Tanzania katika kutoa misaada na mikopo kwa ajili ya miradi mbalimbali ya miundombinu ya barabara, nishati, kilimo, afya, maji, elimu pamoja na maboresho ya sera mbalimbali na kujenga uwezo na aliahidi kuwa Serikali itaendelea kushirikiana na Benki ya Dunia ili kuleta maendeleo nchini. Aidha Katibu Mkuu Kiongozi alimuha kikishia Bibi Bird kuwa Serikali itampa ushirikiano Mkurugenzi Mkazi mpya anayetarajia kuchukua nafasi yake na alisisitiza kuwa suala muhimu ni kuwepo uwazi katika kushughulikia masuala mbalimbali kama ambavyo Bibi Bird amekuwa akifanya. “Nina imani atafuata nyayo zako” alisisitiza Katibu Mkuu Kiongozi.

Mwisho Katibu Mkuu Kiongozi alimtakia Bibi Bird kila la heri katika majukumu yake mapya katika Makao Makuu ya Benki hiyo jijini Washington DC, Marekani.

Katika Kikao hicho Bibi Bird aliongozana na Bibi Prity Arora, ambaye ni Msaidizi wa Mkurugenzi Msaidizi wa Benki ya Dunia nchini. Maafisa wengine waliohudhuria kikao hicho ni Bibi Sauda Nsemo, Kamishna wa Fedha za Nje kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, Bwana Deusdedit Kaganda, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Bwana Fanuel Mathiya, Mratibu Ofisi ya Katibu Mkuu Kiongozi